LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

LHRC

KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

KIJARIDA KUHUSU

# MASHAURI YA NDOA

MAMBO MUHIMU NA KUELEWA KATIKA NDOA NA NAMNA YA KUPELEKA MASHAURI YA NDOA MAHAKAMANI

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*




## Unaweza kutoa taarifa za ukiukwaji wa haki kupitia

# #HakiKiganjani

SMS **0699695486**

Pakua AnroidApp ya **Haki Kiganjani**

hakikiganjani.humanrights.or.tz

***Usipotezee, toa taarifa sasa!***

KIJARIDA KUHUSU

# MASHAURI YA NDOA

MAMBO MUHIMU NA KUELEWA KATIKA NDOA NA NAMNA YA KUPELEKA MASHAURI YA NDOA MAHAKAMANI

**Kimeandaliwa na:**

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu

# YALIYOMO


**SHUKRANI** ........ **5**

**DIBAJI** ........ **7**

**UTANGULIZI** ........ **9**

**1. Maana ya Ndoa** ........ **10**

**2. Aina za Ndoa** ........ **10**

**3. Mambo yanayoweza Kuifanya Ndoa isiwe Halali au Kubatilishwa** ........ **11**

**4. Taratibu za Kufungua Shauri la Ndoa Mahakamani** ........ **12**

4.1.Mambo Yanayoweza Kusababisha Ndoa Ivunjwe ........ 12

4.2.Utaratibu wa kufikisha Masuala ya Ndoa Mahakamani ........ 14

4.3.Hati ya Madai ya Ndoa (Petition) ........ 15

4.4.Matokeo ya Uamuzi wa Mahakama baada ya Kuvunja Ndoa ........ 17

4.5.Mambo Muhimu yanayoangaliwa na Mahakama na pande zote baada ya Kuvunja Ndoa ........ 18

**5. Mgawanyo wa Mali** ........ **19**

**6. Hifadhi na Matunzo ya Watoto** ........ **19**

**7. Rufaa katika Migogoro ya Ndoa** ........ **20**

**8. Kutafuta Tamko la Mahakama** ........ **23**

**9. Matokeo ya Tamko la Mahakama** ........ **24**

**10. HITIMISHO** ........ **24**

## SHUKRANI

Tunatoa shukrani kwa wanasheria wetu na wale wa kujitolea katika uandaaji wa kijarida hiki. Pia tunawashukuru kwa dhati wale wote walioshiriki kwenye kukirejea kijitabu hiki ili kuandaa toleo hili la nne hususan, Wakili Godfrey Mpandikizi, Wakili Joanitha Mutayoba, Wakili Theresia Kinabo, Bi. Irene Nambuo na Bw. Rodrick Maro, pamoja na wafanyakazi wote wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

## UTAMBULISHO WA KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika binafsi la kujitolea na la hiari ambalo si la kisiasa wala kibiashara. Kituo kimeandikishwa na kusajiliwa kwa mujibu wa Sheria za Tanzania mnamo mwezi Septemba, mwaka 1995. Kabla ya kusajiliwa kama chombo huru, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kilikuwa ni mradi wa haki za binadamu wa Mfuko wa Kuendeleza Elimu ya Sheria Tanzania (TANLET). Makao makuu ya Kituo ni Dar es Salaam na Arusha kuna ofisi ndogo.

## MAONO

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taamali jamii yenye haki na usawa.

## TAMKO LA LENGO MAHUSUSI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni shirika lisilo la kiserikali wala kibiashara linalojibidiisha kukuza uwezo wa jamii ili iweze kukuza, kuendeleza na kulinda haki za binadamu na utawala bora nchini Tanzania.

## LENGO KUU

Lengo kuu la Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu ni kukuza uelewa wa sheria na haki za binadamu kwa jamii kwa ujumla na hasa wale wanajamii ambao kwa sababu moja au nyingine wameachwa nyuma. Uelewa unakuzwa kwa njia ya elimu ya uraia na msaada wa kisheria.

# DIBAJI

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina azma ya kusaidia jamii ya Watanzania kuwa na uwezo wa kufahamu sheria za nchi pamoja na kufahamu haki zao ili kuzilinda na kuzitetea pamoja na kuheshimu haki za wengine ili hatimaye tuwe na jamii yenye utamaduni wa kuheshimu haki za binadamu pamoja na nchi inayoheshimu utawala wa sheria.

Tunafahamu kuwa kwa raia wa kawaida si rahisi kuzifahamu sheria zetu zote, na hata baadhi tu ya sheria zinazomgusa kutokana na mfumo tulio nao, ambao hautoi nafasi kwa watu wote kujua sheria. Hali hii inasababisha watu wengi kujikuta katika matatizo ya kisheria ambayo yangeweza kuepukika kama wangejua sheria. Ndiyo maana basi Kituo kimeamua kutoa chapisho hili na mengine, kwa lengo la kwa kutoa msaada wa kisheria kwa raia.

Huu ni usaidizi wa kisheria unaotoa maelezo mafupi na ya msingi ya kisheria ili kukusaidia ndugu msomaji uweze kupata ufumbuzi au maelezo ya tatizo linalokusibu. Ni lengo letu kuwa, katika kijitabu hiki tunatoa usaidizi wa moja kwa moja kwako wewe pale utakapokuwa na tatizo au mmoja wa ndugu au jamaa zako wanapata matatizo ya

namna hii.

Tunachokuomba ni wewe kusoma kwa makini; na pale suala lako linapokwenda mbali zaidi ya maelezo haya, basi utafute msaada wa kisheria au uende kwa mwanasheria aliye karibu na wewe ili aweze kukusaidia.
Tunaamini utapata usaidizi huu kiurahisi zaidi na maelezo yaliyomo humu yatakusaidia kwa karibu. Umalizapo, tafadhali mshirikishe namwenzako kupata usaidizi huu.
Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu.

# UTANGULIZI

Ndoa ni taasisi ya zamani sana katika jamii. Ni taasisi iliyoanza tangu mwanadamu alipoanza kuishi. Kwa kuwa ndoa ndiyo chimbuko la jamii yeyote ile, kila jamii ina utaratibu wa kufuata ili ndoa iwepo na mahusiano yanayotokana na ndoa hiyo yawe mazuri na ya kudumu.

Kutokana na sababu mbalimbali migogoro ya ndoa imekuwa ikijitokeza miongoni mwa wanandoa. Kijitabu hiki kimeandaliwa kwa lengo la kukuza uelewa wa watu kuhusu ndoa na hata taratibu za kufuata ili kupeleka shauri la ndoa mahakamani. Kijitabu hiki kinaeleza kwa ufasaha maana ya ndoa, watu wanaoweza kufunga ndoa, sababu zinazoweza kukubalika mahakamani kuwa ndoa inaweza kuvunjwa, haki ya wanandoa pale ndoa inapovunjika na haki ya watoto pale ndoa inapovunjika.

## 1. MAANA YA NDOA

Kufuatana na sheria ya ndoa ya mwaka 1971, ndoa ni muungano wa hiari wa mwanaume na mwanamke unaokusudiwa kudumu kwa muda wa maisha yao yote.

## 2. AINA ZA NDOA

Ndoa zimagawanyika katika makundi mawili, ndoa ya mke mmoja na ndoa za wake wengi. Makundi haya mawili yamegawanyika katika mifumo ifuatayo:

i. Ndoa za kidini, ambazo zinaweza kuwa za kikristo au kiislamu;
ii. Ndoa za kiserikali;
iii. Ndoa za kimila;
iv. Ndoa inayotokana na dhana kama mwanamke na mwanaume wenye sifa za kufunga ndoa wameishi pamoja mfululizo, kwenye nyumba moja kama mke na mume kwa muda usiopungua miaka 2 au zaidi na jamii inayowazunguka inawachukulia kama mume na mke.

# 3. MAMBO YANAYOWEZA KUIFANYA NDOA ISIWE HALALI AU KUBATILISHWA

i. Kama wahusika hawatakuwa na umri unaokubalika kisheria wa kufunga ndoa,

ii. Kwa ndoa ya mke mmoja, mtu hawezi kuwa na ndoa nyingine;

iii. Watu wenye nasaba moja kama ndugu (maharimu);

iv. Kama mahakama imezuia ndoa isifungwe;

v. Kukiukwa kwa taratibu za ndoa, mf, mfungishaji hana mamlaka kisheria n.k.

vi. Uhanithi;

vii. Wazimu au kifafa cha kurudia rudia rudia;

viii. Kama mwanamke ana ujauzito wa mtu mwingine;

ix. Kama mmoja wa wanandoa atakataa kwa makusudi kufanya tendo la ndoa.

# 4. TARATIBU ZA KUFUNGUA SHAURI LA NDOA MAHAKAMANI

Utaratibu wa kupeleka masuala ya ndoa mahakamani unategemea na jambo linalobishaniwa kwenye ndoa, mambo yanayobishaniwa yanaweza kuwa:-

a. Kutaka ndoa ivunjwe;
b. Kubatilisha ndoa;
c. Kutengana;
d. Matunzo ya watoto na mke;
e. Hifadhi ya watoto;
f. Kutafuta tamko la mahakama.

### 4.1. Mambo Yanayoweza Kusababisha Ndoa Ivunjwe

Ndoa inaweza kuvunjwa na Mahakama iwapo itathibitika kwamba ndoa hiyo imevunjika kiasi ambacho haiwezi kurekebishika tena.

Na hii inaweza kutokana na sababu zifuatazo:-

i. Kama mmoja wa wanandoa amemkimbia mwenzie kwa muda usiopungua miaka mitatu na hajulikani alipo.
ii. Ukatili.
   - Kipigo;
   - Malalamiko yasiyo na msingi;
   - Mume au mke anapomwambukiza

mwenziwe maradhi ya zinaa.

iii. Mmoja kati yao kufungwa maisha au kipindi kirefu kisichopungua miaka 5 au kuwekwa kizuizini.

iv. Uhanithi.

v. Kufanya mapenzi kinyume na maumbile/ kulawiti.

vi. Kulazimisha kufanya tendo la ndoa bila ridhaa ya mwanandoa hasa pale anapokuwa hawezi kufanya hivyo kwa ugonjwa au hali nyingine zinazotambulika

vii. Ugoni.

viii. Uasi/utoro.

ix. Kutengana kwa hiari au kwa amri ya mahakama kwa muda wa miaka mitatu au zaidi.

x. Mume au mke kuwa na ugonjwa wa akili usiotibika, na hii inabidi ithibitishwe na madaktari bingwa wawili wa magonjwa ya akili kuwa mume au mke hatapona tena.

xi. Kubadili dini kwa upande mmoja bila idhini ya upande wa pili endapo pande zote zilikuwa na dini moja.

xii. Dhana ya kifo cha mmoja kati ya wanandoa.

**ANGALIZO:**

Suala la kuugua au kuambukizana magonjwa ya zinaa ikiwemo UKIMWI kati ya mume na mke halijawekwa kama mojawapo ya sababu ya mwanandoa kuweza kudai talaka au kutengana na mwanandoa mwenzie.

### 4.2. Utaratibu wa kufikisha Masuala ya Ndoa Mahakamani

i. Hatua ya kwanza ni kwa mtuanayelalamika kufikisha mgogoro wa ndoa kwenye baraza la usuluhishi la ndoa, ambalo kwa sasa ni baraza la kata au ustawi wa jamii au kwa ndoa za kidini, mabaraza yaliyowekwa na dini husika (mfano Baraza la Walei, Bakwata n.k.);

ii. Baraza likishindwa kutatua mgogoro huo linatoa hati likielezea lilivyoshughulikia suala hilo pamoja na kutoa mapendekezo na maoni yake;

iii. Baadaye mlalamikaji anaweza akapeleka hati ya maombi ya talaka kwenye mahakama anayoona inafaa akiambatanisha hati ya uamuzi wa baraza la usuluhishi la ndoa pamoja na nakala ya hati ya ndoa. Kama

kwenye maombi kuna tuhuma za ugoni yule mlalamikaji anaweza kumshitaki mlalamikiwa pamoja na mke au mume aliyezini naye.

### 4.3. Hati ya Madai ya Ndoa (Petition)

Inatakiwa kuwa na mambo yafuatayo:-

a. Jina la Mahakama;

b. Namba ya shauri na majina ya wahusika;

c. Maelezo ya ndoa yao kuthibitisha kwamba kuna ndoa;

d. Majina, jinsi na umri wa watoto waliozaliwa au kuasiliwa kwenye ndoa kama wapo;

e. Maelezo juu ya mamlaka na uwezo wa Mahakama;

f. Maelezo juu ya shauri lolote/mengine yanayohusiana na ndoa hiyo kama yapo;

g. Maelezo juu ya madai ya msingi yanayoonesha ushahidi kwamba ndoa hiyo imevunjika na haiwezi kurekebishika;

h. Kama mleta maombi hayo amewahi kupatikana na kosa lolote kuhusiana na ndoa hiyo;

i. Makubaliano yanayoonesha kuwepo kwa

matunzo ya watoto au mke na ugawanyaji wa mali au kama hawajafanya makubaliano yoyote basi mleta maombi aeleze mali walizochuma pamoja na anatakiwa atoe mapendekezo yake juu ya mgawanyo wa mali hizo;

j. Maelezo ya nafuu anazoomba;

k. Maombi hayo yaambatane na hati ya uamuzi wa baraza la usuluhishi ambayo imepatikana si zaidi ya miezi sita pamoja na cheti cha ndoa kama kipo.

Hata hivyo kuna masuala ya migogoro ya ndoa ambayo hayahitaji hati ya uamuzi wa Baraza la Usuluhishi, mambo hayo ni:-

i. Kama mlalamikiwa amemkimbia mlalamikaji na hajulikani alipo;

ii. Kama mlalamikiwa anaishi nje ya Tanzania na hatarajii kurudi nchini miezi sita tokea kupelekwa shauri mahakamani;

iii. Kama mlalamikiwa aliitwa kwenye baraza la usuluhishi na kukataa kwa makusudi kuhudhuria;

iv. (iv) Kama mlalamikiwa amefungwa kifungo

cha maisha au kifungo kirefu;

i. (v) Kama mlalamikiwa anaumwa magonjwa ya akili ambayo hayawezi kutibika;

i. (vi) Kama mahakama itaona na kuridhika kwamba mazingira hayamruhusu mlalamikaji kupeleka malalamiko moja kwa moja kwenye Baraza la usuluhishi.

### 4.4. Matokeo ya Uamuzi wa Mahakama baada ya Kuvunja Ndoa

Mahakama ikishasikiliza shauri la ndoa itatoa hukumu kwamba ndoa imevunjwa rasmi. Asiyeridhika na hukumu hiyo ana haki ya kukata rufaa ndani ya siku 45 baada ya kutoka. Baada ya siku 45 kupita, aliyepewa ushindi anatakiwa kuomba utekelezaji wa hukumu kwenye mahakama iliyotoa hukumu.

Hata hivyo ieleweke kwamba ndoa ambayo imevunjwa haitazuia waliokuwa wanandoa kuoana wao wenyewe kwa kufuata utaratibu upya au kuoa na kuolewa na mtu mwingine.

### 4.5. Mambo Muhimu yanayoangaliwa na Mahakama na pande zote baada ya Kuvunja Ndoa

i. Mahakama itakuwa na mamlaka ya kugawa mali zilizochumwa na wanandoa kwa pamoja;

ii. Mahakama inaweza kutoa amri ya kuuzwa kwa mali za wanandoa na kugawanya mali hizo.

Wakati Mahakama inafanya mgawanyo huo itazingatia mambo yafuatayo:-

i. Mila za wanakotoka wahusika;

ii. Kiwango cha mchango wa kila mmoja katika kuchuma mali;

iii. Madeni yoyote yaliyopatikana kwa kukopa mmojawapo kwa manufaa ya wote;

iv. Kama kuna watoto.

**ANGALIZO**

Mahakama haipokei maombi ya kuvunja ndoa endapo ndoa husika haijadumu kwa miaka miwili au zaidi labda mwombaji aonyeshe taabu au shida anazopata kutokana na kuendelea na ndoa.

## 5. MGAWANYO WA MALI

Kisheria mahakama inatakiwa kugawa mali zilizochumwa kwa pamoja. Katika kufanya uamuzi huo kila mmoja anatakiwa kuthibitisha kwamba mali hizo zimechumwa pamoja.

Mahakama inapogawa mali inazingatia pamoja na mambo mengine mchango wa kila mmoja na vile vile wanandoa wanaweza kuwa na mali zao binafsi ambazo zitabakia ni mali za mmiliki wake na hazitagawiwa kama mali zilizochumwa kwa pamoja na mke na mume. Mchango wa mke katika kuchuma mali ni pamoja na kazi za ndani ambazo zinafanywa na mke wakati ndoa inaendelea.

## 6. HIFADHI NA MATUNZO YA WATOTO

Mahakama itatoa uamuzi wa hifadhi ya watoto na ni nani awajibike kuwatunza. Hii itazingatia ustawi wa watoto. Watoto wenye umri chini ya miaka 7 huamuliwa kuhifadhiwa na mama zao lakini kama mahakama

itaridhika kwamba mtoto atakaa kwa ustawi zaidi anapohifadhiwa na baba au mtu mwingine inaweza kuamuru atunzwe na mtu huyo.  Suala la matunzo ya watoto ni jukumu la baba lakini kama baba hana uwezo au hayupo mama atawajibika kutunza mtoto/ watoto.  Watoto wenye umri zaidi ya miaka 7 wana uwezo wa kutoa maoni wapi wanataka kukaa na maoni yao yatazingatiwa. Mahakama huzingatia maslahi makuu ya watoto hivyo hata kama mama hana uwezo wa kifedha baba atatakiwa atoe fedha/matunzo ili mtoto aishi na mama yake.

## 7. RUFAA KATIKA MIGOGORO YA NDOA

Kama mwanandoa hajaridhika na uamuzi wa mahakama utaratibu ufuatao uzingatiwe katika kukata rufaa:

a. Mwanandoa ambaye hajaridhika na uamuzi wa mahakama anaweza kuwasilisha rufaa yake kwa kuandika sababu za rufaa kwenye hati ya rufaa na kuwasilisha mahakama ya juu ndani ya siku 45 tokea siku ya maamuzi.

b. Rufaa inaweza kuandikwa kwa Kiswahili au Kiingereza.

Hati iliyopelekwa ya sababu za rufaa inaweza kusikilizwa bila kujali kwamba ina mapungufu ya kisheria katika uandaaji. Ni muhimu hati ya rufaa ikaambatanishwa na nakala yua hukumu na mwenendo wa shauri linalokatiwa rufaa.

» **Kubatilisha ndoa**:

Kama itagundulika kwamba ndoa ilifungwa bila kufuata taratibu zilizowekwa kisheria, mlalamikaji halazimiki kwenda kwanza Baraza la usuluhishi.

Mfano: mlalamikiwa alikuwa na mimba ya mtu mwingine, ana maradhi ya zinaa au kama mwanamke alikuwa na umri chini ya miaka 18 na wazazi wake hawakutoa ridhaa inavyotakiwa kisheria.

Madhara au matokeo yake ni kama ndoa haikufungwa na vitu vyote halali vilivyofanywa wakati wa ndoa hiyo vitakuwa batili isipokuwa mtoto au watoto waliozaliwa ndani ya ndoa.

» **Kutengana:**

Kutengana kunaweza kufanywa kwa hiari kati ya mke na mume pale ambapo hawakusudii kuvunja ndoa yao na wanapeana nafasi ya kujisahihisha au kwa njia ya kwenda mahakamani kwa kufuata utaratibu ufuatao:-

i. Ombi la kuomba amri ya kutengana kutoka mahakamani hufikishwa mahakani moja kwa moja bila kupitia baraza la usuluhishi la ndoa.

ii. Mahakama inapotoa amri ya kutengana inaweza kuamuru matunzo ya watoto au mke yatolewe na mume. Pia ikumbukwe kwamba ombi la matunzo ya watoto au mke linaweza kupelekwa mahakamani hata kama hakuna ombi la kuvunja ndoa endapo mume hawajibiki kutunza au amewatelekeza mke na mtoto au watoto.

Vilevile inazingatiwa kwamba katika kutoa ombi la hifadhi na matunzo mahakama inaangalia zaidi hali ya ustawi wa mtoto kwa atakaye amriwa kumhifadhi.

iii. Mahakama huangalia matakwa ya wazazi wa mtoto.

Endapo mtoto anaweza kutoa maamuzi sahihi matakwa ya mtoto yatazingatiwa pia.

iv. Mila na desturi za wazazi wa watoto nazo huzingatiwa.

## 8. KUTAFUTA TAMKO LA MAHAKAMA

Mtu yeyote ambaye ana sababu ya msingi au sababu za msingi kutaka ndoa iliyofungwa itenguliwe anaweza kupeleka maombi maalumu ya kutaka ndoa hiyo itenguliwe endapo ndoa hiyo inavunja sheria za ndoa za Tanzania, kama vile ndoa ya wanandugu, n.k.

Kama ndoa imewahi kuvunjwa au kubatilishwa kisheria na mahakama za nchi nyingine, mtu yeyote anaweza kupeleka ombi mahakamani kuomba tamko la kutengua na kusajili hati ya talaka.

## 9. MATOKEO YA TAMKO LA MAHAKAMA

Matokeo ni kutenguliwa kwa ndoa hiyo na hivyo ndoa hiyo inakuwa batili isipokuwa watoto waliozaliwa ndani ya ndoa hiyo.

Ikumbukwe: Kwamba mahakama zote isipokuwa mahakama ya rufaa zina uwezo sawa kusikiliza mashauri ya ndoa.

## 10. HITIMISHO

Msomaji wetu, ni matumaini yetu kwamba mpaka sasa unajua maana ya ndoa na jinsi ya kufungua na kuendesha mashauri ya ndoa mahakamani. Kutengana huwa inakuwa ni kwa muda fulani tu na inaweza kuwa ni kwa amri ya mahakama au ridhaa ya wanandoa. Pia tumeona kuwa ni lazima shauri lipitie baraza la usuluhishi kabla ya kupelekwa mahakamani. Ni muhimu kuzingatia hili kwani hati ya kuomba kuvunja ndoa haitasikilizwa bila kuambatanishwa na hati ya baraza la usuluhishi, labda tu kutokana na mazingira yaliyoainishwa hapo juu ambapo hati ya baraza sio muhimu.

**KITUO CHA SHERIA NA HAKI ZA BINADAMU**
S. L. P. 75254, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu:** +255 22 2773038/48 **Nukushi:** +255 22 2773037
**Barua Pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**DODOMA OFFICE**
Kitalu na 22. Area D,
S.L.P 2289, Dodoma, Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 262350050
**Barua pepe:** lhrc@humanrights.or.tz

**Ofisi ya Arusha**
Barabara ya Olerian, Olosiva Kitalu Na. 116/5,
Sakina kwa Idd, Arumeru
S. L. P. 15243, Arusha - Tanzania
**Simu:** +255 27 2544187
**Barua Pepe:** lhrcarusha@humanrights.or.tz

**Kituo cha Msaada wa Sheria**
Mtaa wa Isere - Kinondoni
S. L. P. 79633, Dar es Salaam - Tanzania
**Simu/Nukushi:** +255 22 2761205/6
**Barua Pepe:** legalaid@humanrights.or.tz

@humanrightstz HakiTV

*Kwa Jamii yenye Haki na Usawa*